

Toleo la. 13

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKLEZA | APEWE TENA 5 | 12 SEPTEMBER, 2020



*HUKU DKT. MAGUFULI
KULE DKT. MWINYI
...HATOKI MTU!*



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**



MAGUFULI KUWANEEMESHA WAFUGAJI NCHINI

• Kutengeneza Ajira Kupitia Ufugaji

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli, katika kipindi cha miaka mitano ijayo itaendeleza mageuzi makubwa na ya kisayansi katika sekta ya mifugo ili kuongeza tija, ajira na kuinua mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa.

Kwa mujibu wa Ilani ya CCM, Serikali chini ya Rais Magufuli itatenga maeneo ya ufugaji, itarahisisha upatikanaji wa maji, itakuza uzalishaji wa vyakula vya mifugo viwandani sambamba na kuongeza idadi ya maafisa ugani.

Katika muhula wake pili, Dkt. Magufuli atatenga maeneo ya ufugaji kwa kuyatambua, kuyapima, kuyasajili na kuyamilikisha ili kuongeza maeneo yaliyotengwa kutoka hekta milioni 2,788,901.17 hadi hekta milioni 6,000,000 jambo litakalosaidia kuondoa migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Sambamba na hilo, Serikali itarahisisha upatikanaji wa maji kwa kuongeza mabwawa na mabwawa ya maji ya mifugo kutoka 1,384 hadi 1,842 na kuongeza visima kutoka 103 hadi 225 ili kurahisisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika maeneo ya wafugaji.

Aidha, Serikali ya CCM itaongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo viwandani kutoka tani 900,000 mwaka 2020 hadi tani milioni 8 mwaka 2025 pamoja na kuongeza uzalishaji wa mazao yatokanayo na mifugo ikiwemo maziwa kutoka lita bilioni 2.7 hadi wastani wa lita bilioni 4.5, nyama nyekundu kutoka wastani wa tani 690,629 hadi tani 790,000, nyama nyeupe kutoka tani 82,500 hadi tani 150,000, mayai kutoka bilioni 3.6 hadi bilioni tano na ngozi kutoka tani 16 hadi 25 kwa mwaka.

Pamoja na hayo, Serikali ya Awamu ya Tano itaongeza idadi ya Maafisa Ugani kwa kuhakikisha kuwa kila kata na kijiji kinafikiwa na Afisa Ugani au mtoa huduma za ugani, jambo litakalotoa fursa ya ajira kwa wahitimu wa vyuo vya kilimo sambamba na kuhakikisha sekta ya ufugaji inakua zaidi.

Mbali na hayo, CCM imedhamiria kwa dhati kuongeza upatikanaji wa huduma muhimu kama maji, afya na elimu kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji kutulia sehemu moja na kuwaepusha na kadhia ya kuhamahama kufuata huduma hizo.





MAJALIWA: CHAGUENI KIONGOZI ATAKAYELINDA AMANI

Na Mwandishi Maalum - **TANGA**

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amewataka wanananchi wa Tanga na watanzania kwa ujumla wahakikishe ifikapo Oktoba 28, mwaka huu wanajitokeza kwa wingi kwenda kumchagua kiongozi mwenye uwezo wa kulinda tunu mbalimbali za Taifa ikiwemo amani na Muungano.

“Wana-Tanga bila ya kujali itikadi za vyama nipo hapa mbele yenu kwa unyenyekevu mkubwa, nawaomba ifikapo Oktoba 28 mwaka huu tumchague Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ili akaendeleze miradi ya maendeleo aliyoianzisha. Pia nawaomba tumchague Ummu Mwalimu katika nafasi ya ubunge katika jiji letu la Tanga pamoja na wagombea wa udiwani wa CCM,” ameeleza Mhe. Majaliwa wakati akimuomba kura Rais Majugufuli, Ummu Mwalimu na Madiwani, katika mkutano uliofanyika viwanja vya Tangamano, Tanga.

Amewataka wanananchi kumchagua Dkt. Magufuli kwa sababu ni kiongozi shupavu mwenye uwezo wa kufanya maamuzi na asiyekubali kuyumbishwa na yeyote. Pia Rais Dkt. Magufuli ni kiongozi mwenye kuwajali watanzania na atakayewaruhusu waendeleo kuabudu kwa uhuru na ndio maana hata uchaguzi umepangwa kufanyika siku ya Jumatano ili kutoa fursa kwa wanananchi kutumia siku za Ijumaa, Jumatosi na Jumapili kwa ajili ya ibada.

Kuhusu ujenzi wa barabara katika jiji hilo, Mhe. Majaliwa amesema shilingi bilioni 66.8 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga-Pangani yenye urefu wa kilometa 50. “Shilingi bilioni 2.3 katika uwekaji wa taa za barabarani 436 kwa barabara zilizopo ndani ya Jiji la Tanga na taa za kuongoza magari katika barabara ya Mombasa. Ujenzi wa miundombinu hii umeinua uchumi wa wanananchi wa Jiji la Tanga kwa kuwawezesha kufanya kazi zao bila vikwazo,” alieleza.

Amesema shilingi bilioni 21.9 zimetumika kuboresha barabara zenye urefu wa kilometa 16.4 kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ni barabara ya Sita na barabara ya Chumbageni, Barabara ya Nne na Chumbageni hadi Ikulu, Barabara ya kutoka Diwani/Ikulu, Taifa na Sahare Phase I.

Barabara zingine ni barabara ya kutoka Diwani hadi Mwabonde, barabara ya Mabawa-Msambweni I, barabara ya kutoka Mabawa, barabara ya Nguvumali, barabara ya Nane na Jamatcan, barabara ya Msambweni na Barabara ya stendi ya Kange.

Mhe. Majaliwa amesema shilingi bilioni

2.2 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa mifereji mikubwa ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 3.44 jijini Tanga. Pia shilingi bilioni 10 zimetumika kuboresha miundombinu ya barabara kwa kiwango cha changarawe na udongo katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Amesema katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Halmashauri ya jiji la Tanga imepanga kutumia shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mabawa-Msambweni II na barabara ya 11 na ya 12 kwa kiwango cha lami, ambapo kwa sasa utekelezaji wake upo katika hatua za awali.





MWINYI ANATOSHA NAFASI YA URAIS ZANZIBAR - DKT. SHEIN

Na Mwandishi Wetu - **ZANZIBAR**

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, amesema mgombea wa kiti cha Urais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ana sifa zote za kuchaguliwa kushika nafasi hiyo ili aweze kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar kwa kasi zaidi.

Dkt. Shein ameyasema hayo leo wakati wa uzinduzi wa kampeni za Mgombea wa Urais Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi uliofanyika katika Uwanja wa Demokrasia uliopo Kibanda Maiti mijini Zanzibar na kueleza kuwa mgombea huyo ana uwezo mkubwa wa kuongoza kutokana na uzoefu na weledi alionao.

"Zanzibar inatakiwa kuongozwa na mtu asiye na madaha, mwebwe wala majivuno bali mtu mpenda maendeleo na mwenye uwezo na uzoefu wa kutosha katika masuala ya uongozi kama alivyo Dkt. Mwinyi", ameeleza Dkt. Shein.

Sambamba na hilo, Dkt. Shein amewaomba wazanzibari wote wasifanye makosa ya kumchagua anayejaribu uongozi bali wamchague Dkt. Hussein Ali Mwinyi ili aendelee kazi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Saba ya Mapinduzi Zanzibar.

"Dkt. Hussein Ali Mwinyi atashirikiana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kudumisha Muungano wetu na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar", Alisisitiza Rais Dkt. Shein.

Fauka ya hayo, Dkt. Shein amesema kuwa mgombea huyo wa CCM hatakuwa na mzaha katika suala la kulinda amani, umoja na mshikamano kwa sababu amefanikiwa kuyasimamia mambo hayo katika nyadhifa mbalimbali alizowahi kushika.



DKT. MWINYI: NIMEDHAMIRIA KUWATUMIKIA NA KULINDA MASLAHI YA WAZANZIBARI

Na Mwandishi Mahususi - ZANZIBAR

Mgombea Urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) Dkt. Hussein Ali Mwinyi ameomba ridhaa ya kuongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa dhamira ya kuwatumikia na kulinda maslahi ya wazanzibari wote.

Ameyasema hayo leo katika uwanja wa Demokrasia uliopo Kibanda Maiti mjini Zanzibar ambapo ameahidi kufanya kazi kwa uadilifu na kuwashughulikia wote wanaofanya kazi kwa mazoea wakiwemo walarushwa, wezi, wazembe na wabadhilifu kwani watakuwa kikwazo katika kufanikisha malengo ya ilani ya CCM ya mwaka 2020 - 2025.

“Tutakuza sekta ya utalii na kuongeza watalii wanaokuja hapa Zanzibar hadi kufikia 850,000 hivyo tutazalisha ajira nyingi, tutapanua bandari yetu iwe ya kisasa zaidi ili kuweza kupokea meli nyingi zaidi zikiwemo zinazoleta watalii, tutajenga miundombinu ya barabara za lami zaidi ya kilomita 198 Pemba na Unguja,” Ameeleza Dkt. Mwinyi.

Kuhusiana na ajira, amefahamisha kuwa Serikali itazalisha fursa nyingi kupitia uanzishwaji wa viwanda, kukuza sekta ya uvuvi kwa kutoa zana za kisasa kwa wavuvi, na kuendeleza mazao ya karafuu na mwani ili kuzalisha ajira.

Pamoja na hayo, Dkt. Mwinyi ameahidi kulinda rasilimali za Zanzibar zikiwemo mafuta na gesi ili ziwanufaishe wananchi wote sambamba na kuchangia katika kuboresha utoaji wa huduma za jamii.

“Tutaimarisha zaidi huduma za jamii kama Sekta ya Maji kuanzia pale Serikali ya Awamu ya Saba ilipoishia, kuimarisha huduma za afya zikiwemo za kibingwa”, amefahamisha Dkt. Mwinyi.

Sambamba na hayo, Dkt. Mwinyi amesema Serikali yake itashughulikia kwa nguvu zote tatizo la madawa ya kulevya ili kulinda rasilimali watu kwa maslahi mapana ya taifa.

Mbali na hayo, Dkt. Mwinyi amesema kuwa ataendeleza sera ya CCM ya Muungano wa Serikali mbili na kuzilinda tunu za Muungano na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

5 KALI ZA CHAMA CHA MAPINDUZI

Sekta ya Ufugaji

01

Serikali imeongeza maeneo ya ufugaji kutoka hekta milioni 1.4 mwaka 2015 hadi hekta 5.0 mwaka 2020 na maeneo ya malisho yenye jumla ya hekta 2,788,901.17 yalitengwa kwa ajili ya ufugaji katika Mikoa 22.

02

Viwanda vya kusindika maziwa viliongezeka kutoka 82 mwaka 2015 hadi viwanda 99 mwaka 2020, viwanda vya kusindika nyama viliongezeka kutoka 25 mwaka 2015 hadi viwanda 33 mwaka 2020. Aidha, viwanda 9 vya ngozi ambavyo vimesaidia usindikaji wa ngozi wa hatua ya kati kufikia futi za mraba 124,420,000 kwa

03

Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, Serikali imejipanga kuendelea kubainisha na kutenga maeneo ya ufugaji kwa kuyatambua, kuyapima, kuyasajili na kuyamilikisha ili kuongeza maeneo yaliyotengwa kutoka hekta 2,788,901.17 hadi hekta 6,000,000.

04

Katika Ilani ya CCM ya mwaka 2020- 2025, Serikali imejipanga kuongeza malambo na mabwawa ya maji ya mifugo kutoka 1,384 hadi 1,842 na visima 103 hadi 225 ili kurahisisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo.

05

Katika Ilani ya CCM ya mwaka 2020- 2025, Serikali imejipanga kuboresha afya ya mifugo nchini kwa kuimarisha kinga, chanjo na tiba na kuhakikisha chanjo za ruzuku kwa magonjwa 13 ya kipaumbele na kuhakikisha kila Hal-mashauri inakuwa na mfumo baridi wa kutunzia chanjo za mifugo.



MBINGA WAMUAHIDI MAGUFULI USHINDI WA KISHINDO

Na Mwandishi Maalum - RUVUMA

Wakazi wa wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wameahidi kumpa ushindi wa kishindo Rais Dkt. John Pombe Magufuli na mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa maendeleo makubwa aliyoyaleta wilayani humo katika muhula wake wa kwanza.

Wakizungumza na jarida hili wilayani Mbinga leo, wananchi hao akiwemo Alex Komba amesema kuwa Rais Dkt. Magufuli amefanya mapinduzi makubwa katika sekta za miundombinu, afya, elimu na maji ukiwamo ujenzi wa barabara ya Mbinga-Nyasa iliyojengwa kwa kiwango cha lami katika maeneo korofi hali inayorahisisha usafirishaji.

“Magufuli ni mkombozi wetu katujengea barabara, na pia leo watoto wetu wanasoma bila kulipa ada kuanzia shule ya msingi hadi Sekondari, vituo vya afya na zahanati alizojenga zimetuwezesha kupata huduma zote hapahapa, hata upasuaji unafanyika tofauti na zamani ambapo tulikuwa tukiteseka kufuata huduma mbali”, ameeleza.

Sambamba na hayo, Komba amesema wakazi wa wilaya hiyo wanaunga mkono dhamira ya Serikali ya Awamu ya tano kujenga vituo vya afya vya kisasa ambavyo vimezuia vifo vya wakinamama na watoto hivyo Magufuli ana kila sababu ya kuchaguliwa tena kuiongoza Tanzania ifikapo Oktoba 28, 2020.

Kwa upande wake Anacletus Mhagama ambaye ni mkazi wa Mbinga anasema kwa sasa wananchi walio wengi wanajua kuchambua pumba na mchele na kwamba hawako tayari kuyumbishwa na wanasiasa waongo wanotoa ahadi zisizotekelezeka na zinazolenga kuwanufaisha mabeberu.

“Kujengwa kwa miundombinu ya elimu na uchukuzi kunawawezesha wananchi kufurahia matunda ya kodi wanazolipa kwani Rais Magufuli amehakikisha fedha zote zinazokusanywa nchini zinatumiwa kwa maslahi ya Watanzania,” ameeleza. Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 imejikita katika kuimarisha huduma za jamii zikiwemo barabara, elimu, afya, na upatikanaji wa maji safi na salama.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**